TANGAZO LA SERIKALI Na. 521 la tarehe 28/6/2024

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE GARI MOJA INC KWA AJILI YA MRADI WA HESHIMU BAHARI (RESPECT THE OCEAN) LINALOINGIZWA NCHINI NA CHEMONICS INTERNATIONAL INC YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa Kwenye Gari moja Kwa Ajili ya Mradi wa Heshimu Bahari (Respect the Ocean) Linaloingizwa Nchini na Chemonics International Inc ya Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika kuanzia tarehe 3 Mei, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa gari lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii lililoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha na Chemonics International Inc kwa ajili ya Mradi wa "Heshimu Bahari (Respect the Ocean)" unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa gari hilo litatumika kwa matumizi mengine, mbali na matumizi yaliyoainishwa katika Amri hii au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafikia ukomo tarehe 3 Septemba, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Chesesi | Namba ya injini |
|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA LANDCRUISER PRADO TXL, TURBO DIESEL, 7-SEATER, 5 DOORS | JTEBR9FJ40K319503 | 1GD-9197430 |

Dodoma,
12 Juni, 2024.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*